# NISHATI
HABARI ZA NISHATI

# News Bulletin

www.nishati.go.tz | Wizara ya Nishati | wizara_ya_nishati_tanzania | @Nishati2017 | Wizara ya Nishati

Toleo Namba 49 — Aprili 1 - 30, 2023


## DIRA YA TAIFA YA KUHAMIA KATIKA

# NISHATI SAFI YA KUPIKIA KUZINDULIWA MWEZI JUNI



*Waziri Wa Nishati, Mhe. January Makamba*


**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
**Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma**



# BODI YA UHARIRI


**Mwenyekiti**
**Mhandisi Felchesmi Mramba**
Katibu Mkuu

**Makamu Mwenyekiti**
**Kheri Mahimbali**

**Mhariri**
**Dorina G. Makaya**

**Waandishi**

Teresia Mhagama
Zuena Msuya
Hafsa Omar
Timotheo Mathayo

**Msanifu Kurasa**

Lucas Gordon





**Wasiliana nasi kwa simu namba** +255-26-2322018
**Nukushi:** +255-26-2320148
au

**Fika Ofisi ya Mawasiliano**
Mitumba Dodoma,
S.L.P 2494, Dodoma

*www.nishati.go.tz*
*Wizara ya Nishati*
*@Nishati2017*
*wizara_ya_nishati_tanzania*
*Wizara ya Nishati*

# DIRA YA TAIFA YA KUHAMIA KATIKA NISHATI SAFI YA KUPIKIA KUZINDULIWA MWEZI JUNI





*Waziri Wa Nishati, Mhe. January akitoa elimu ya nishati safi ya kupikia kwa Wajumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) pamoja na Wenyeviti na Makatibu wa UWT wa Mikoa na Wilaya, Machi 21, 2023 jijini Dodoma.*

**Na Teresia Mhagama**

Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba ameeleza kuwa, mwezi Juni mwaka huu utafanyika uzinduzi wa kitaifa wa Dira ya Taifa ya kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia na Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Dira hiyo ambayo itaainisha masuala mbalimbali ikiwemo hatua ambazo Serikali itachukua ili kuwezesha asilimia 80 ya watanzania kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2033.

Waziri Makamba aliyasema hayo tarehe 21 Machi, 2023 jijini Dodoma wakati akitoa elimu ya nishati safi ya kupikia kwa Wajumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) pamoja na Wenyeviti na Makatibu wa UWT wa Mikoa na Wilaya ambao watasadia kulipa msukumo suala hilo na kusambaza elimu husika katika ngazi ya Kata na Matawi nchi nzima.



*Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Mary Chatanda akizungumza na Wajumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) pamoja na Wenyeviti na Makatibu wa UWT wa Mikoa na Wilaya, Machi 21, 2023 jijini Dodoma.*



*Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Tanzania Bara, Ndg. Abdulrahman Kinana akizungumza na Wajumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) pamoja na Wenyeviti na Makatibu wa UWT wa Mikoa na Wilaya, Machi 21, 2023 jijini Dodoma.*

"Takwimu zinaonesha kuwa, asilimia Nane tu ya watanzania ndio wanatumia nishati safi ya kupikia hivyo, Mhe. Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatoa maelekezo kuwa ndani ya miaka 10 asilimia 80 ya watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia, ameshatuelekeza tutengeneze Dira, Mkakati na Mwelekeo na pia

# DIRA YA TAIFA YA KUHAMIA KATIKA NISHATI SAFI YA KUPIKIA KUZINDULIWA MWEZI JUNI





*Wajumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) pamoja na Wenyeviti na Makatibu wa UWT wa Mikoa na Wilaya, wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (hayupo pichani) wakati akitoa elimu ya nishati safi ya kupikia Machi 21, 2023 jijini Dodoma.*

kuanzisha mfuko wa nishati safi ya kupikia ili kuweka ruzuku itakayowawezesha wananchi wa kipato cha chini kumudu bei ya gesi, hii ni kazi kubwa lakini inawezekana na kazi inaendelea." Amesema Makamba.

Alieleza kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita imeamua kulivalia njuga suala la nishati safi ya kupikia ikiwa ni moja ya jitihada zake za kuboresha maisha ya watanzania hasa kinamama.

Makamba alisema kuwa, ustawi wa mwanamke wa Tanzania unahatarishwa na namna anavyotafuta nishati na aina ya nishati anayopikia, "Wataalam wanasema lisaa limoja jikoni ni sawa na sigara 300 sasa hapa unategemea ustawi utatoka wapi?, bahati nzuri Mhe.Rais ameliona hili na kwa Wizara ya Nishati, suala Nishati ya kupikia ni jambo namba moja la kutekeleza ili kuleta ustawi ulio bora nchini."



*Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Dk. Philis Nyimbi akizungumza na Wajumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) pamoja na Wenyeviti na Makatibu wa UWT wa Mikoa na Wilaya, Machi 21, 2023 jijini Dodoma.*

Aliwaeleza Wajumbe hao pia athari mbalimbali zinazotokana na matumizi ya nishati chafu ya kupikia kama vile kuni ambapo alitaja athari hizo kuwa ni pamoja na magonjwa katika mfumo wa upumuaji, mazingira hatarishi wakati wa kutafuta kuni, wanyama hatarishi na athari katika masomo kwa watoto wa kike kwani badala ya kutumia muda mrefu kusoma, muda mwingi wanautumia kutafuta kuni kwa ajili ya kupikia.

Katika kuhakikisha kuwa, kazi hiyo ya uhamasishaji wa nishati safi ya kupikia inafanyika kwa ufanisi, Waziri Makamba alitoa mitungi 400 ya gesi ya kupikia kwa UWT kila mkoa nchini pamoja mitungi 1500 kwa UWT Makao Makuu ili waweze kuitumia katika uhamasishaji wa nishati safi ya kupikia katika maeneo yao.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa UWT, Mary Chatanda amlimshukuru Waziri wa Nishati kwa kutoa elimu hiyo ambayo Wajumbe hao wataitumia kuhamasisha matumizi ya nishati safi katika ngazi za chini.

Mgeni rasmi katika Mkutano huo alikuwa ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Tanzania Bara, Ndg. Abdulrahman Kinana.

# MRADI WA KUFUA UMEME WA KAKONO KUANZA

## >>> Shilingi Bilioni 750 za kuendeleza mradi zasainiwa

**Na Zuena Msuya, Dar es Salaam,**




*Mkurugenzi Mkaazi wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) Celine Robert( kushoto) na Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Mwigulu Nchemba wakisaini mkopo wa fedha za kuwezesha utekelezaji wa Mradi wa kufua umeme wa Maji wa Kakono kuwezesha mkopo wa fedha za utekelezaji wa Mradi wa kufua umeme wa Maji wa Kakono hafla iliyofanyika Machi 15, 2023, Jijini Dar es Salaam, kulia anayeshuhudia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum. (kulia), jijini Dar es Salaam.*

Mradi wa kufua umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera (Kakono) wenye uwezo wa MW 87.8 utaanza kutekelezwa hivi karibuni baada ya kusainiwa kwa mkopo wa Dola za Marekani Milioni 325 sawa na shilingi Bilioni 750 za Kitanzania kati ya Serikali ya Tanzania na Mashirika ya Kimataifa ya Maendeleo.

Hayo yalielezwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Mwigulu Nchemba wakati wa hafla ya utiaji saini mkopo huo iliyofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Fedha na Mipango jijini Dar es Salaam, Machi 15, 2023.




*Meneja Mkaazi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) nchini Tanzania, Dkt. Patricia Laverley (kushoto) na Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt.Mwigulu Nchemba wakionyesha nyaraka za saini ya mkopo wa fedha za kuwezesha utekelezaji wa Mradi wa kufua umeme wa Maji wa Kakono, hafla iliyofanyika Machi 15, 2023, jijini Dar es Salaam. Kulia anayeshuhudia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum. (kulia), jijini Dar es Salaam.*

Alisema kuwa, fedha hizo zimetolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ambayo imetoa Dola za Marekani milioni 161.47 sawa na shilingi 374.9 Bilioni, Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) limetoa Euro Milioni 110 sawa na takriban shilingi 272.6 Bilioni na Umoja wa Ulaya (EU) umetoa Euro milioni 35 sawa na shilingi 86.7 Bilioni.

Aliongeza kuwa, katika fedha hizo Serikali itatoa Dola za Marekani Milioni 6.03 sawa na takribani shilingi Bilioni 13 za Kitanzania ili kuhakikisha mradi huo unatekelezwa ndani ya kipindi cha miaka mitano kama ilivyopangwa.

Dkt.Nchemba alisema kuwa mradi wa Kakono unaendana na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III) na sehemu ya ajenda pana ya Serikali ya Awamu ya Sita inayolenga kujenga Uchumi wa Kiushindani na uchumi wa Viwanda kwa Maendeleo ya Watu kwa kuboresha miundombinu yenye tija, upatikanaji wa nishati ya uhakika, kuimarisha mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji pamoja na mifumo ya elimu na mafunzo.

“Kufuatia hatua hii muhimu iliyofikiwa, naomba kuhamasisha

# MRADI WA KUFUA UMEME WA KAKONO KUANZA

maandalizi ya mkataba wa Umoja wa Ulaya uharakishwe ili kuwa na fedha zote za ufadhili tayari kwa utekelezaji wa mradi", alisema Mwigulu. Aliongeza kusema kuwa mkataba uliobaki kusainiwa ni mmoja tu wa Umoja wa Ulaya ambapo kwa Upande wake Serikali ya Tanzania iko tayari kufanya hivyo.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Edson Ngabo alisema lengo kuu la Mradi huo ni kuongeza uzalishaji wa nishati kwenye Gridi ya Taifa kutokana na vyanzo vya gharama nafuu na




*Mhandisi Edson Ngabo kutoka Wizara ya Nishati, akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, baada ya kusainiwa kwa mkopo wa fedha za kutekeleza wa Mradi wa kufua umeme wa Maji wa Kakono, hafla iliyofanyika Machi 15, 2023, Jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt.Mwigulu Nchemba (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Saada Nkuya, (wa pili kulia mtari wa mbele), Washirika wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Maendeleo la Ufaransa na Umoja wa Ulaya na Viongozi waandamizi kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi zake, Wizara ya Fedha na Mipango na maofisa wengine wa Serikali wakati hafla iliyofanyika Machi 15, 2023, jijini Dar es Salaam.*

pia kuongeza uhakika wa umeme katika maeneo ya Kaskazini-Magharibi mwa Tanzania hususani mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Alifafanua kuwa utekelezaji wa mradi huo utakamilika ndani ya miaka mitano (5) na utahusisha ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa MW 87.8, njia ya kusafirishia umeme, kuboresha Kituo cha kupoza umeme na kazi nyingine zikiwemo ujenzi wa shule ya msingi na kituo cha afya katika maeneo ambayo mradi utatekelezwa.

Vilevile ujenzi wa barabara ya lami yenye urefu wa kilomita 28 na hivyo kuboresha hali ya maisha ya jamii ya kanda hiyo na pia unahusisha usambazaji wa umeme na utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa mazingira na kijamii.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Saada Nkuya, Washirika wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Maendeleo la Ufaransa na Umoja wa Ulaya na viongozi waandamizi kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi zake, Wizara ya Fedha na Mipango na maofisa wengine wa Serikali.

# NAIBU WAZIRI WA NISHATI AZINDUA MPANGO WA MIAKA MINNE WA MASUALA YA JINSIA WA TANESCO

**Na Reuben Richard**

Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato amezindua Mpango wa miaka minne wa masuala wa jinsia wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ambao utawezesha masuala mbalimbali ikiwemo kuboresha mfumo wa upatikanaji na utoaji wa takwimu za jinsia katika Shirika hilo.

Uzinduzi huo ulifanyika tarehe 30/3/2023 jijini Dodoma na kuhudhuriwa na viongozi na wadau mbalimbali wakiwemo Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO, Mhe. Balozi Mwanaidi Majaar na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande.



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizungumza wakati wa hafla ya kuzindua Mpango wa Miaka Minne wa Masuala ya Jinsia wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) iliyofanyika jijini Dodoma*

“Tumezindua programu hii ambayo itahamasisha na kusimamia haki na usawa wa watu wote katika eneo la kazi na mwisho wa siku tunataka TANESCO iwe mfano wa mashirika mengine katika kusimamia na kutekeleza masuala ya jinsia.”alisema Byabato




*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka akizungumza wakati wa hafla ya kuzindua Mpango wa Miaka Minne wa Masuala ya Jinsia wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) iliyofanyika jijini Dodoma.*

Alisema kuwa, katika mpango huo masuala mbalimbali yatakayofanyika ni pamoja na kuwa na sera ya Taasisi ambayo itaelekeza mambo mengi ikiwemo utaratibu kuwajengea uwezo vijana wa kike ili waweze kuingia katika kazi za kitaalam ambapo utaratibu huo utahusisha kuwatoa vijana katika vyuo na kuwapeleka kwenye Shirika na kuwapa mafunzo na baadaye kupewa ajira.

Jitihada nyingine zitakazofanyika ni kuhakikisha nafasi mbalimbali katika shirika zina wanawake na vijana wa kike sawa na wanaume sambamba na kuwapeleka shule ili waongeze uelewa na ujuzi utakaowawezesha kumudu nafasi mbalimbali shirikani.

Ili mpango huo wa jinsia ufanyike kwa ufanisi, Naibu Waziri aliiagiza TANESCO kuanzisha kitengo maalum kitakachokuwa kikishughulikia masuala ya jinsia katika Shirika hilo ikiwemo malalamiko yanayohusu jinsia.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande alisema kuwa, suala la usawa wa kijinsia linapewa kipaumbele na TANESCO na tayari Shirika hilo limeshaweka mikakati ya kuhakikisha wanaongeza viongozi na wafanyakazi wanawake katika Shirika na kwamba Bodi pamoja na Wizara ya Nishati inawaunga mkono katika suala hilo.

“Katika utekelezaji wa suala hili la usawa wa kijinsia TANESCO tumebahatika kwani kwenye mradi wa TAZA ambao unalenga kusafirisha umeme kutoka Tanzania hadi Zambia, moja ya matakwa yake ni utekelezaji wa suala la usawa wa kijinsia, bahati nzuri suala hilo linaenda na mpango mkakati wa TANESCO hivyo sasa tunaanza safari ya kutekeleza suala hilo ili kupunguza mwanya wa usawa wa kijinsia katika Shirika.” Alisema Chande




*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizindua Mpango wa Miaka Minne wa Masuala ya Jinsia wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakati wa hafla ya kuzindua mpango huo iliyofanyika jijini Dodoma. Wa Nne kutoka Kulia ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka, Wa Tatu kulia ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO, Mhe.Balozi Mwanaidi Maajar na wa Tatu kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (wa Tatu kutoka kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande wakizindua nembo ya Mpango wa Miaka Minne wa Masuala ya Jinsia wa TANESCO wakati wa hafla ya kuzindua mpango huo iliyofanyika jijini Dodoma. Wa kwanza Kulia ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka na wa Pili kulia ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO, Mhe.Balozi Mwanaidi Maajar.*






*Wadau mbalimbali wakiwa katika hafla ya kuzindua Mpango wa Miaka Minne wa Masuala ya Jinsia wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) iliyofanyika jijini Dodoma.*

# SERIKALI, WFP, UNCDF KUWEZESHA 80% YA WATANZANIA KUTUMIA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

**Zuena Msuya Dodoma**

Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la Chakula Duniani (WFP), Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo ya Mitaji (UNCDF) na wadau wengine wa maendeleo ndani na nje ya nchi wanafanya jitihada mbalimbali ili kuwezesha asilimia 80 ya Watanzania kutumia nishati safi ya kupikia ndani ya kipindi cha miaka kumi kuanzia sasa.

Hayo yalielezwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba wakati akifungua Kongamano la siku mbili la Nishati Safi ya kupikia lililoandaliwa na WFP na UNCDF ambalo limelenga kuzikutanisha pamoja Serikali, Sekta Binafsi na wadau wa maendeleo ili kwa pamoja waweze kufanikisha azma ya Serikali ya kuwezesha watanzania kuhama kutoka kwenye nishati isiyo safi ya kupikia na kutumia nishati safi ya kupikia.

Mramba alisema kuwa, hatua hiyo ni utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 1 Novemba 2022 wakati wa ufunguzi wa Mjadala kuhusu Nishati safi ya kupikia, kuwa asilimia 80% ya watanzania wanatakiwa kutumia




*Mkurugenzi Mkazi na Mwakilishi wa Shirika la Chakula Duniani nchini Tanzania, Bi.Sarah Gibson akizungumza wakati wa kongamano la Nishati Safi ya Kupikia lililofanyika jijini Dodoma ambalo lilihusisha wadau mbalimbali zikiwemo Taasisi za Serikali na Wadau wa Maendeleo.*




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba akizungumza wakati wa kongamano la Nishati Safi ya Kupikia lililofanyika jijini Dodoma ambalo lilihusisha wadau mbalimbali zikiwemo Taasisi za Serikali na Wadau wa Maendeleo.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (kulia, mbele) na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga (kushoto, mbele) wakiwa katika kongamano la Nishati Safi ya Kupikia lililofanyika jijini Dodoma ambalo lilihusisha wadau mbalimbali zikiwemo Taasisi za Serikali na Wadau wa Maendeleo.*



*Wataalam kutoka Wizara ya Nishati, wakiwa katika kongamano la Nishati Safi ya Kupikia lililofanyika jijini Dodoma ambalo lilihusisha wadau mbalimbali zikiwemo Taasisi za Serikali na Wadau wa Maendeleo.*

# SERIKALI, WFP, UNCDF KUWEZESHA 80% YA WATANZANIA KUTUMIA NISHATI SAFI YA KUPIKIA




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (katikati waliokaa), Mkurugenzi Mkazi na Mwakilishi wa Shirika la Chakula Duniani nchini Tanzania, Bi.Sarah Gibson (wa Pili kulia waliokaa) na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga (wa kwanza kulia waliokaa) wakiwa katika picha ya pamoja na wadau waliohudhuria kongamano la Nishati Safi ya Kupikia lililofanyika jijini Dodoma.*

nishati safi ya kupikia ndani kipindi cha miaka 10.

Aliongeza kuwa, Mhe.Rais pia alielekeza kuanzishwa kwa kikundi kazi cha kusimamia ishati safi ya kupikia na kutengeneza mpango mkakati wa miaka kumi wenye sheria,utaratibu na kanuni zitakazotumika katika nishati safi ya kupikia ambapo Kikundi kazi hicho kinaendelea na kazi husika.

"Katika kutekeleza na kufanikisha watanzania kutumia nishati safi ya kupikia, Serikali inashirikiana na wadau mbalimbali kama vile sekta binafsi, wagunduzi na wavumbuzi, wadau wa nishati ya kupikia ili kuhakikisha mipango yote iliyowekwa na Serikali inafanikiwa, na sasa tuko katika hatua za kukamilisha mpango mkakati wa miaka kumi wa kuangalia taratibu na sheria zinazokinzana ili wote tuzungumze lugha moja." alisema Mhandisi Mramba.

Aliongeza kuwa, kwa sasa kumekuwa na mwitiko mkubwa wa wanasiasa pamoja na viongozi mbalimbali katika ngazi ya Mikoa, Wilaya na Vijiji katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkaazi na Mwakilishi wa Shirika la Chakula Duniani (WFP), Sarah Gibson, alisema kuwa shirika hilo litashirikiana na Serikali ya Tanzania kuhakikisha kuwa mipango iliyojiwekea ya watanzania kutumia nishati safi ya kupiikia inafanikiwa.

Naye, Meneja katika Taasisi ya Umoja wa Mataifa inayosimamia Maendeleo ya Mitaji (UNCDF), Imanuel Muro alisema taasisi hiyo inatoa mitaji kwa wafanyabiashara ili waweze kufanya biashara ya bidhaa za nishati safi ya kupikia kwa kuwapa masharti ya kupunguza bei ya bidhaa zao ili watumiaji wazipate kwa urahisi na kwa bei nafuu.




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (katikati waliokaa), Mkurugenzi Mkazi na Mwakilishi wa Shirika la Chakula Duniani nchini Tanzania, Bi.Sarah Gibson (wa Pili kulia waliokaa) na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga (wa kwanza kulia waliokaa) wakiwa katika picha ya pamoja na wataalam Kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi zake waliohudhuria kongamano la Nishati Safi ya Kupikia lililofanyika jijini Dodoma.*

# MAJADILIANO MRADI WA KUCHAKATA NA KUSINDIKA GESI ASILIA (LNG) YAKAMILIKA

**Na Teresia Mhagama**

Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba, amesema kuwa, majadiliano yanayohusu Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia baina ya Serikali ya Tanzania na wawekezaji Kampuni ya Shell ya Uholanzi na Equinor ya Norway na washirika wao yamekamilika na kwamba sasa wataalam wapo katika kazi ya kuandika mikataba ya mradi huo.

Waziri wa Nishati aliyasema hayo tarehe 06 Machi, 2023 jijini Arusha wakati akitoa vipaumbele vya Wizara katika Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati ambapo pamoja na masuala mengine ya kiutumishi, Baraza hilo limepitia Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Nishati kwa mwaka 2023/2024.

"Mazungumzo ya mradi huu wa LNG yamekamilika na wataalam kwa sasa wanaandika mikataba mikubwa miwili yenye masuala mengi ikiwemo ya kiufundi, Mkataba mmoja ni wa Nchi Hodhi (HGA) na mwingine ni mkataba uliounganishwa wa vitalu vya Gesi Asilia Namba I,II na IV ambavyo gesi yake itatumika kwenye mradi wa LNG, kila mkataba una kurasa zaidi ya 600, hii si kazi ndogo ila nimewasisitiza wamalize kazi mwezi huu ili kuweza kuendelea na hatua nyingine za utekelezaji." Amesema Makamba

Alisema kuwa mradi huo ambao uwekezaji wake ni zaidi ya Shilingi Trilioni 70 utaleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi nchini na utaifanya Tanzania kuwa moja ya nchi zinazochangia katika usalama wa nishati duniani hivyo amewataka Watendaji wa Wizara ya Nishati kuendelea kusimamia utekelezaji wa mradi huo.

Makamba alitaja mradi mwingine unaoendelea kutekelezwa ni wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania ambapo kwa sasa shughuli mbalimbali za maandalizi ya ujenzi zinaendelea na mwezi uliopita Serikali imetoa kibali cha ujenzi wa bomba hilo kwa kampuni ya EACOP na kwa sasa inaendelea kukamilisha taratibu za kupata pesa za kutekeleza mradi huo ambazo zimefikia mwishoni.

Aliongeza kuwa, zoezi la ulipaji fidia kwa watu 9800 katika mkuza wa Bomba la mafuta zinaendelea ambapo mpaka sasa shilingi Bilioni 29.2 zimelipwa kati ya shilingi Bilioni 30 zilizokuwa zinahitajika kwenye ulipaji fidia na matarajio ni kwamba ujenzi unatarajiwa kuanza kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Alitaja baadhi ya faida zitakazotokana na mradi huo kuwa ni pamoja na ajira 10,000, Serikali kupata mapato kupitia tozo ya kupitisha mafuta, ada mbalimbali kupitia matumizi ya Bandari ya Tanga na kampuni mbalimbali za kitanzania zitatoa huduma katika mradi huo. Pia ujenzi wa bomba unahamasisha shughuli za utafiti na uchimbaji wa mafuta kwani linapita kwenye maeneo yenye viashiria vya upatikanaji wa mafuta hivyo Tanzania ikipata mafuta tayari miundombinu ya usafirishaji mafuta hayo ipo.

Kuhusu hali ya upatikanaji umeme alisema kuwa, kazi ya kurekebisha miundiombinu na kuongeza uzalishaji umeme inaendelea kupitia miradi mbalimbali kama ya gridi imara na hivi karibuni Serikali imesaini mikataba ya takriban ya shilingi Trilioni 1.9 ya kurekebisha miundombinu ya umeme. Amesema kuwa, kazi hiyo inachukua muda hivyo amewaomba watanzania wawe na subira ili matunda ya uwekezaji kama huo yaonekane.

Kuhusu Nishati Safi ya Kupikia, alisema kuwa






*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizungumza katika Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati jijini Arusha ambapo pamoja na masuala mengine, Baraza hilo lilipitia Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Nishati kwa mwaka 2023/2024.*

# MAJADILIANO MRADI WA KUCHAKATA NA KUSINDIKA GESI ASILIA (LNG) YAKAMILIKA

hiyo ni ajenda ya Wizara ya Nishati kwani ni suala linalowagusa watanzania wote kuanzia mtu maskini hadi tajiri hivyo Serikali ambayo ina jukumu la kuboresha maisha ya watanzania inalisimamia suala hilo ili nchi iingie kwenye nishati safi ya kupikia huku akitolea mfano nchi ya India ambayo asilimia 98 ya wananchi wake hawatumii kuni na mkaa .

"Kamati inayohusika na mradi huu wa Nishati Safi ya Kupikia inafanya kazi na kabla ya Bajeti ya Mwaka 2023/2024, Serikali itatoa Dira, Mkakati na Mwelekeo wa kuondokana na matumizi ya nishati chafu na isiyo salama kwa takriban asilimia 80 ndani ya miaka 10, na haya ni maelekezo ya Mhe,Rais hivyo lazima tuyatekeleze." Ameeleza Makamba

Katika hatua nyingine, Makamba aliwataka watendaji wa Wizara kubuni vyanzo vya mapato vya kutekeleza miradi ya Nishati na kutoitegemea Serikali pekee hivyo amewaelekeza watendaji hao kushirikisha sekta binafsi ili kutekeleza miradi ya nishati.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato alimshukuru Waziri wa Nishati kwa ubunifu wa miradi mbalimbali itakayoboresha Sekta ya Nishati nchini na kwamba chini ya uongozi wake tayari kuna mafanikio yanaonekana na kuahidi kuwa watendaji wa Wizara wataendelea kufanya kazi kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba alimshukuru Waziri kwa jitihada mbalimbali na msukumo anaoutoa katika Sekta ya Nishati nchini ikiwemo suala la uwepo wa Nishati Safi ya Kupikia na kusema kuwa Watumishi na viongozi wa Wizara watafanya kila jitihadi ili kutekeleza miongozo anayoitoa.

Akifunga Mkutano huo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Athuman Mbuttuka alisema kuwa masuala yote yaliyoelekezwa na Viongozi Wakuu wa Wizara yatafanyiwa kazi na kwamba kuna kazi kubwa ya kutekeleza masuala hayo, pia amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kumteua kuhudumu katika Sekta ya Nishati na pia amesisitiza uwepo wa ushirikiano katika kutekeleza masuala mbalimbali ya Wizara.




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, akizungumza katika Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati jijini Arusha ambapo pamoja na masuala mengine, Baraza hilo lilipitia Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Nishati kwa mwaka 2023/2024.*



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Athuman Mbuttuka akifunga Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi Wizara ya Nishati jijini Arusha, tarehe 6 Machi, 2023.*




*Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (katikati) na viongozi wengine wa Wizara wakiimba Wimbo wa Wafanyakazi wa Mshikamano kabla ya kufungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati jijini Arusha. Wa Tatu kutoka kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Wa Tatu kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Wa Pili kushoto ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athuman Mbuttuka na wa kwanza kulia ni Katibu wa Baraza la Wafanyakazi Wizara ya Nishati, Fortunata Getele.*



*Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba (katikati) akiwa katika picha ya pamoja Menejimenti ya Wizara ya Nishati mara baada ya kufungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati jijini Arusha. Wa Tatu kutoka kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Wa Tatu kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Wa Pili kushoto ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athuman Mbuttuka. Wa kwanza kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Bahati Mtono, Wengine ni Katibu wa TUGHE Taifa, Meshack Lugeiyamu na Katibu wa Baraza la Wafanyakazi Wizara ya Nishati, Fortunata Getele.*



*Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba (katikati) akiwa katika picha ya pamoja Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi Wizara ya Nishati, mara baada ya kufungua Mkutano wa Baraza hilo jijini Arusha. Wa Tatu kutoka kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Wa Tatu kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Wa Pili kushoto ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athuman Mbuttuka. Wa kwanza kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Bahati Mtono, Wengine ni Katibu wa TUGHE Taifa, Meshack Lugeiyamu na Katibu wa Baraza la Wafanyakazi Wizara ya Nishati, Fortunata Getele.*



*Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba (katikati) akiwa katika picha ya pamoja sekretarieti ya Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi Wizara ya Nishati, mara baada ya kufungua Mkutano wa Baraza hilo jijini Arusha. Wa Tatu kutoka kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Wa Tatu kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Wa Pili kushoto ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athuman Mbuttuka. Wa kwanza kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Bahati Mtono, Wengine ni Katibu wa TUGHE Taifa, Meshack Lugeiyamu na Katibu wa Baraza la Wafanyakazi Wizara ya Nishati, Fortunata Getele.*



*Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati wakiwa katika Mkutano wa Baraza uliofanyika jijini Arusha ambapo pamoja na masuala mengine, Baraza hilo lilipitia Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Nishati kwa mwaka 2023/2024.*

# DOLA BILIONI 1.9 KUIMARISHA GRIDI YA TAIFA NCHINI

**Na Timotheo Mathayo, Dodoma.**

Waziri wa Nishati, January Makamba amesema kuwa Serikali imetenga fedha kiasi cha Dola za Marekani bilioni 1.9 kwa ajili ya miradi ya kuimarisha gridi ya Taifa kwa kipindi cha miaka minne.

Makamba alisema hayo wakati wa uwasilishaji wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2022/2023 kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Jijini Dodoma, Machi 23, 2023.

"Katika Mwaka wa fedha 2022/2023 mradi huu umetengewa sh. Bilioni 500 kwa lengo la kufanya usanifu wa mradi, kupata wakandarasi, kununua vifaa na kuanza utekelezaji wa mradi," alisema Makamba.

Waziri Makamba amefafanua kuwa mradi huo unahusisha ununuzi na ufungaji wa mashine umba 6,000, kusimika nguzo 380,000 za umeme, kununua na kufunga nyaya zenye urefu wa kilomita 46,200 za kusambaza umeme, kununua na kufunga mita za LUKU 700,000.

Alisema fedha hiyo itawezesha kujenga njia za kusafirisha umeme zenye urefu wa kilomita 948 zenye msongo wa kV 132 na kV 22, kujenga vituo 14 vya kupoza umeme wa 220/33 kV na 132/33 kV pamoja na kununua na kufunga mashine umba 66 za ukubwa wa MVA 50, MVA 60, MVA 90 na MVA 120.

"Serikali kupitia mradi huu kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) imefanikiwa kuunganisha Mkoa wa Kigoma katika Gridi ya Taifa kupitia kituo cha Nyakanazi pamoja na kuunganisha Wilaya ya Ngara na Biharamulo kupitia kituo hicho hicho cha Nyakanazi," alisema Makamba.

Uthamini wa mali za Wananchi watakaopisha ujenzi wa miradi ya umeme imefanyika kwa mradi wa Tabora - Katavi, Tabora - Kigoma, Shinyanga -Simiyu na uthamini unaendelea kwa miradi ya Benako - Kyaka, Songea - Tunduru - Masasi, Kiyungu - Rombo, Kasiga - Lushoto, Mkata - Kilindi, Pugu - Mkuranga na Bunda - Ukerewe.

"Tathimini ya athari za mazingira imekamilika kwa miradi ya Tabora - Katavi, Tabora - Urambo na Mabibo - Kinyerezi. Kwa miradi ya Benako - Kyaka, Shinyanga – Simiyu na Ilala – Kurasini taarifa ya athari za kimazingira tayari imewasilishwa Baraza la mazingira nchini (NEMC) ili kupata vyeti," amesema Makamba.

Kwa Miradi iliyobaki ya Songea-Tunduru, Tunduru- Masasi, Kiyungu-Rombo,Kisiga-Lushoto, Mkata- Kilindi,Pugu-Mkuranga,Kibaha-Zegereni na Bunda- Ukerewe tathmini ya athari ya mazingira imeanza kufanyika.

Kamati hiyo ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeishauri Wizara kuongeza usimamizi katika utekelezaji wa Miradi ya umeme nchini.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athumani Selemani Mbuttuka, wajumbe wa Bodi kutoka taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Nishati, Wakurungezi kutoka taasisi hizo pamoja na watendaji wengine kutoka Wizara na taasisi.



*Waziri wa Nishati, January Makamba akizungumza jambo wakati wa uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 kwa wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Machi 23, 2023 jijini Dodoma.*



Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula akiongoza kikao wakati Wizara ya Nishati ilipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa kipindi cha mwaka 2022/2023.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (wa kwanza kushoto) akiwa na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (wa kwanza kulia) pamoja na Mkurugenzi wa Shirika la umeme Tanzania, Maharage Chande (Katikati), wakiwa kwenye kikao cha kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa kipindi cha mwaka 2022/2023.



Wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini pamoja na Watendaji walioshiriki kikao cha kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa kipindi cha mwaka 2022/2023.





Baadhi ya watendaji wa Wizara ya Nishati na watendaji kutoka taasisi zilizopo chini ya Wizara walioshiriki kikao cha kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa kipindi cha mwaka 2022/2023.

# UJENZI WA NJIA YA KUSAFIRISHA UMEME KATIKA MRADI WA JNHPP YAFIKIA ASILIMIA 92



*Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (wa kwanza kushoto) akieleza jambo wakati Wizara ya Nishati ilipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini jijini Dodoma.*

**Na Timotheo Mathayo, Dodoma.**

Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba amesema kuwa, Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) inaendelea na utekelezaji wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Bwawa la Julius Nyerere hadi Chalinze pamoja na ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme cha Chalinze ambapo ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya kV 400 imefikia asilimia 92.

Makamba alisema hayo Machi 12, 2023 wakati Wizara ya Nishati ilipotoa taarifa ya utekelezaji wa Mradi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Bwawa hilo la kuzalisha umeme hadi Chalinze kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini jijini Dodoma.

"Utekelezaji wa miradi hii ipo katika hatua mbalimbali, mradi wa njia ya kusafirisha umeme yenye msongo wa kilovoti 400 imefikia asilimia 92 na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze ambacho kinahusisha ufungaji wa Mashine umba sita umefikia asilimia 55." Alisema Makamba

Alifafanua kuwa, mradi huo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) ambapo njia hiyo ya kusafirisha umeme ina urefu wa kilomita 160 na ujenzi wa Kituo cha kupoza Umeme cha Chalinze



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Dunstan Kitandula (wa kwanza kushoto) akiongoza kikao cha Kamati hiyo wakati Wizara ya Nishati ilipowasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa wajumbe wa kamati hiyo.*

# UJENZI WA NJIA YA KUSAFIRISHA UMEME KATIKA MRADI WA JNHPP YAFIKIA ASILIMIA 92

inahusisha ufungaji wa Transfoma Sita.

"Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, gharama ya mradi ni Dola za Marekani milioni 51.5 na shilingi bilioni 39.12 ambapo ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme utatumia kiasi cha Dola za Marekani Milioni 44.06 na Shilingi Bilioni 30.85 zinatumika kwa ajili ya kujenga kituo cha kupoza umeme cha Chalinze," Alisema Makamba.

Alitaja Mkandarasi wa mradi wa kusafirisha umeme kuwa ni Larsen & Toubro Limited kutoka India na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze unatekelezwa na Mkandarasi TBEA kutoka China.



*Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (wa pili kushoto) akiwasilisha taarifa ya Muundo wa Wizara ya Nishati kwa wajumbe wa kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini jijini Dodoma.*



*Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Mhe. Judith Kapinga akifuatilia taarifa mbalimbali kutoka kwa watendaji wa Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zake wakati wa uwasilishaji wa utekelezaji wa miradi mbalimbali kwenye kamati hiyo ya Bunge.*

Mwenyekiti wa kamati hiyo ya Bunge, Mhe..Dunstan Kitandula aliipongeza Serikali kwa jitihada ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Sekta ya Umeme, Gesi na Mafuta ikiwemo mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta ghafi la Afrika Mashariki.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga na watendaji wengine kutoka Wizara ya Nishati, Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

Mkuranga,Kibaha-Zegereni na Bunda - Ukerewe tathmini ya athari ya mazingira imeanza kufanyika.


Kamati hiyo ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeishauri Wizara kuongeza usimamizi katika utekelezaji wa Miradi ya umeme nchini.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athumani Selemani Mbuttuka, wajumbe wa Bodi kutoka taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Nishati, Wakurungezi kutoka taasisi hizo pamoja na watendaji wengine kutoka Wizara na taasisi.

# KATIBU MKUU WIZARA YA NISHATI AFANYA MAZUNGUMZO NA BALOZI MPYA WA JAPAN NCHINI



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba akiwa katika kikao na Balozi wa Japan nchini Tanzania Yasushi Misawa (wa Tatu kulia) kilichofika katika Ofisi za Wizara ya Nishati jijini Dodoma. Wa Pili kutoka kushoto ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka. Wengine katika picha ni watendaji kutoka Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha na Mipango na Ubalozi wa Japan nchini Tanzania.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Balozi wa Japan nchini Tanzania Yasushi Misawa (wa Pili kushoto) na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka (wa kwanza kushoto) mara baada ya kumaliza kikao chao jijini Dodoma. Wengine katika picha ni watendaji kutoka Wizara ya Fedha na Mipango na Ubalozi wa Japan nchini Tanzania.*

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amekutana na kufanya mazunguzo na Balozi Mpya wa Japan nchini Tanzania, Yasushi Misawa kuhusu kuendelea kushirikiana katika miradi mbalimbali ya Nishati nchini.

Mazungumzo hayo yalifanyika Machi 13, 2023 katika ofisi za Wizara ya Nishati jijini Dodoma.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka pamoja na Viongozi wengine waandamizi kutoka Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha na Ubalozi wa Japan nchini.

Katika mazungumzo hayo, Mramba aliishukuru Serikali ya Japan kwa kuendelea kushirikiana na Tanzania kutekeleza miradi mbalimbali ya nishati ukiwemo wa kuhamasisha matumizi ya Gesi Asilia.

Alisema, Tanzania ipo tayari kuendeleza ushirikiano na Japan katika kutekeleza miradi ya Nishati.


Kwa upande wake, Balozi wa Japan nchini Tanzania, Yasushi Misawa alimueleza Katibu Mkuu huyo kuwa amekuja Wizara ya Nishati ili kujitambulisha na kueleza kuwa Japan itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kutekeleza miradi mbalimbali inayoendelea ikiwepo ya kuhamasisha matumizi ya Gesi Asilia, kuzalisha umeme kutokana na Nishati Jadidifu hasa Upepo na ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Aliongeza kuwa, Japan imeendelea kushirikiana na Tanzania katika kutekeleza miradi mbalimbali katika Sekta ya Elimu, Afya, Maji, pamoja Ujenzi wa miundombinu.

Baadhi ya miradi ya umeme ambayo inatekelezwa kwa ushirikiano wa nchi hizo mbili ni pamoja na njia ya kusafirisha umeme ya msongo mkubwa wa Kilovolti 400 katika mradi wa Backbone na vituo vya Kupoza na Kusambaza Umeme katika maeneo mbalimbali nchini.



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (Wa Sita kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Balozi wa Japan nchini Tanzania Yasushi Misawa (wa Tano kutoka kushoto) na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka (wa Nne kushoto) mara baada ya kumaliza kikao chao jijini Dodoma. Wengine katika picha ni watendaji kutoka Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha na Mipango na Ubalozi wa Japan nchini Tanzania.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Balozi wa Japan nchini Tanzania Yasushi Misawa (katikati) na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka (kushoto) mara baada ya kumaliza kikao chao jijini Dodoma.*



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka, ( katikati) akitoa maelekezo wakati wa kikao cha kikundi kazi cha wataalamu katika mradi wa Nishati Safi ya Kupikia kilichokutana kwa siku tatu kuanzia tarehe 13 hadi 20, 2023, jijini Dodoma.*

# NAIBU KATIBU MKUU NISHATI AONGOZA KIKAO CHA KIKUNDI KAZI CHA TAIFA CHA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

**Na Zuena Msuya, Dodoma**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka ameongoza kikao cha wataalam wa Kikundi Kazi cha Taifa cha Nishati Safi ya Kupikia ili kupitia taarifa mbalimbali zilizoandaliwa na sekretatieti ya kikundi kazi hicho ikiwemo Dira ya taifa ya kuhamia katika matumizi ya nishati safi kupikia na Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Dira hiyo.

Kikundi Kazi hicho kilikutana kwa siku tatu kuanzia tarehe 18 hadi 20 Machi, 2023, jijini Dodoma.

Mbuttuka alisema Kikundi kazi hicho kinaandaa Dira ya Taifa ya Kuhamia katika Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia 2033; Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Nishati Safi ya Kupikia 2033; na Muundo wa Mfuko wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia kwa kuainisha kazi, wajibu, muundo na vyanzo vya fedha.

Kikosi kazi hicho pia kinaandaa rasimu ya katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa kila taasisi inayolisha watu zaidi ya mia tatu (300) ifikapo mwaka 2024 na watu mia moja (100) hadi mia tatu (300) ifikapo mwaka 2025.

Aliongeza kuwa, Kikosi kazi hicho kinapitia na kufanya uchambuzi wa



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka, ( katikati) akizungumza katika kikao cha kikundi kazi cha wataalamu katika mradi wa Nishati Safi ya Kupikia kilichokutana kwa siku tatu kuanzia tarehe 13 hadi 20, 2023, jijini Dodoma.*

# NAIBU KATIBU MKUU NISHATI AONGOZA KIKAO CHA KIKUNDI KAZI CHA TAIFA CHA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

Sera, Mipango na Mikakati mbalimbali iliyopo na kupendekeza maboresho stahiki yatakayohakikisha uwepo wa miongozo yenye utengamano utakaopelekea uendelevu na uwepo wa mazingira wezeshi ya uwekezaji katika sekta ya nishati safi ya kupikia.

Kikundi Kazi hicho kinajumuisha maafisa waandamizi kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge, Sera na Uratibu), Wizara ya Nishati, Wizara ya Madini, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Wizara ya Kilimo pamoja na Taasisi zinazohusika.

Ikumbukwe kwamba Katika ufunguzi wa Mjadala wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia 2022, tarehe 1 Novemba 2022, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo mbalimbali katika hotuba yake. Mojawapo ya maelekezo hayo ni kuundwa kwa Kikundi Kazi cha Taifa kitakachojumuisha Serikali, Sekta Binafsi na Wadau wa Maendeleo kwa ajili ya kusimamia masuala yote yanayohusika na nishati safi ya kupikia nchini.

Kikundi kazi hicho kiliundwa na kuanza utekelezaji wa majukumu Mwezi Novemba, 2022.





*Baadhi ya wajumbe wa kikundi kazi cha wataalamu katika mradi wa Nishati Safi ya Kupikia kilichokutana kwa siku tatu kuanzia tarehe 13 hadi 20, 2023, jijini Dodoma.*

# WAWEKEZAJI KUTOKA UGANDA WAONYESHA NIA YA KUWEKEZA KATIKA MIRADI YA UMEME TANZANIA

**Na Zuena Msuya, Dodoma**

Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba amekutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Uganda nchini Tanzania pamoja na wawekezaji kutoka nchini humo ambao walimweleza Waziri nia yao ya kuwekeza katika miradi mbalimbali ya umeme ukiwemo wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Lindi, Masasi, Tunduru na Songea.

Mazungumzo hayo yalifanyika Machi 21, 2023 katika ofisi za Wizara ya Nishati jijini Dodoma na kuwashirikisha Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka, Kamishna Msaidizi Maendeleo ya umeme, Mhandisi Styden Rwebangila na wawekezaji kutoka Uganda.

Wawekezaji hao walimueleza Waziri Makamba kuwa wanataka kuwekeza katika mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa Msongo mkubwa wa Kilovolti 400 wenye urefu wa Kilometa 222.3 kutoka Lindi, Masasi hadi Songea.

Walisema kuwa watawekeza katika kusanifu, kutafuta fedha, kujenga na kuendesha njia hiyo na kuikabidhi baada ya muda uliopangwa wataikabidhi njia hiyo kwa TANESCO.

Waziri Makamba pamoja na kueleza kuwa, Serikali inawakaribisha wawekezaji kama hao, aliwaagiza kukutana na Shirika la Umeme nchini na maafisa wa Wizara ya Nishati ili kujadiliana na kuona njia bora ya kutekeleza mradi huo kwa kuangalia sheria, taratibu na kanuni za uwekezaji katika miradi ya umeme.

Aidha Wawekezaji hao pia walionyesha nia ya kutaka kuwekeza katika mradi wa umeme wa jua katika Kisiwa cha Mafia wenye megawati 5.



*Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba(kulia) akiwa mazungumzo na Balozi wa Uganda nchini Tanzania, Col Mwesigye Fred (kushoto) na wawekezaji kutoka Uganda kuhusu kuwekeza katika mradi wa umeme, Machi 21, 2023. Wa pili kulia ni Naibu Katibu Mkuu Wizaya ya Nishati, Athumani Mbuttuka.*

Hata hivyo Waziri aliwaeleza wawekazaji hao kuwa Serikali imeshapata kiasi cha Dola za Kimarekani Milioni 5 kutoka Wakala wa Maendeleo wa Ufaransa (AFD) na kwamba iko katika mazungumzo ya AFD kuongeza fedha zaidi za kutekeleza mradi huo.

Kwa upande wake Balozi wa Uganda nchini Tanzani, Col. Mwesigye Fred aliishukuru Serikali ya Tanzania, kwa kukubali wawekezaji kutoka nchi Uganda kuwekeza katika miradi ya umeme.

Alisema hayo ni matokeo ya ushirikiano mzuri kati ya nchi hizo mbili ulioasisiwa na viongozi wakuu.



*Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba(kushoto) akizungumza na Balozi wa Uganda nchini Tanzania, Col Mwesigye Fred (wa pili kushoto) na wawekezaji kutoka Uganda kuhusu kuwekeza katika mradi wa umeme, Machi 21, 2023. Wa pili kulia ni Naibu Katibu Mkuu Wizaya ya Nishati, Athumani Mbuttuka.*



*Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba (nne kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Balozi wa Uganda nchini Tanzania, Col Mwesigye Fred (wa tatu kulia), Katibu Mkuu Wizaya ya Nishati, Athumani Mbuttuka( wa tatu kushoto), Kamishna Msaidizi Maendeleo ya umeme, Mhandisi Styden Rwebangila(kushoto) na wawekezaji kutoka Uganda kuhusu kuwekeza katika mradi wa umeme, Machi 21, 2023. Wa pili kulia ni Naibu.*

# DKT. YONAZI AONGOZA KIKAO CHA MAKATIBU WAKUU CHA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

**Na Zuena Msuya, Dodoma**

Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) Dkt. Jim Yonazi ameongoza Kikao cha Kamati ya Uongozi ngazi ya Makatibu Wakuu kilicholenga kupitia utekelezaji wa maboresho ya rasimu ya Dira ya Taifa ya kuhamia katika matumizi ya Nishati safi ya kupikia 2033 na rasimu ya Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Nishati Safi ya Kupikia 2033 yaliyotolewa na Waziri Mkuu wiki moja iliyopita Machi 23, 2023 Mkoani Dodoma.

Dkt.Yonazi aliongoza Kikao hicho kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi ngazi ya Makatibu Wakuu ambaye ni Katibu Mkuu Kiongozi.

Kikao hicho kilihusisha Makatibu Wakuu kutoka Wizara mbalimbali akiwemo Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka na Wajumbe wa Kikundi Kazi cha Taifa cha Nishati Safi ya Kupikia kilichofanyika Machi 30, 2023 Jijini Dodoma.

Dkt. Yonaz alisema kuwa kikao hicho ni mahsusi kwa ajili ya kupitia utekelezaji wa maboresho na maelekezo yaliotolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipokutana na Mawaziri na Naibu Mawaziri Machi 23, 2023 Mkoani Dodoma.

Mara baada ya Makatibu Wakuu hao kupitia Rasimu ya Dira ya Taifa ya kuhamia katika matumizi safi ya Nishati Safi ya Kupikia 2033 na Rasimu ya Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Nishati Safi ya Kupikia, itawasilishwa kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.





*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka (katika), Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) Dkt. Jim Yonazi(kulia),Katibu Mkuu ofisi ya rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa( TAMISEMI), Adolf Ndunguru wakiwa katika Kikao cha Makatibu Wakuu cha nishati safi ya kupikia wakipitia utekelezaji wa maboresho ya rasimu ya Dira ya Taifa ya kuhamia katika matumizi ya Nishati safi ya kupikia 2033 na rasimu ya Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Nishati Safi ya Kupikia 2033, kilichofanyika Machi 30, 2023 Jijijini Dodoma.*



*Wajumbe wa Kikao cha Makatibu Wakuu cha nishati safi ya kupikia, wakipitia utekelezaji wa maboresho ya rasimu ya Dira ya Taifa ya kuhamia katika matumizi ya Nishati safi ya kupikia 2033 na rasimu ya Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Nishati Safi ya Kupikia 2033, wakimsikiliza kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi ya Makatibu Wakuu Katibu, ambaye pia ni Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) Dkt. Jim Yonazi, kilichofanyika Machi 30, 2023 Jijijini Dodoma.*



*Baadhi ya Wajumbe Sekretarieti ya Kikundi Kazi cha Taifa cha Nishati Safi ya Kupikia wakimsikiliza Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi ya Makatibu Wakuu Katibu, ambaye pia ni Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) Dkt. Jim Yonazi, kilichofanyika Machi 30, 2023 Jijijini Dodoma.*




*Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba akizungumza na Umoja wa Wafanyabiashara wa Gesi za Mitungi ya Majumbani nchini (TZLPGA) wakati akizundua umoja huo uliofanyika Machi 15, 2023 jijini Dar es Salaam.*

# SERIKALI YAUNGA MKONO WASAMBAZAJI WA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

**Na Zuena Msuya, Dar es Salaam**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amesema kuwa, Serikali inaendelea kuunga mkono juhudi za Sekta Binafsi katika kuhakikisha watanzania wote wanatumia nishati safi ya kupikia ili kutimiza azma ya Serikali ya kuhakikisha asilimia 80 ya watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia hadi kufikia mwaka 2034.

Alisema hayo wakati akizindua Umoja wa Wafanyabiashara wa Gesi za Mitungi ya Kupikia nchini (TZLPGA), Machi 15, 2023 jijini Dar es Salaam.

Mramba aliwapongeza wafanyabiashara hao kwa kuanzisha umoja huo kwakuwa watakuwa wakiweka mipango ya pamoja kuhakikisha kuwa watanzania wote wanatumia nishati safi ya kupikia kwa vile wao ndiyo wadau wakubwa wa kusambaza gesi za mitungi kwa matumizi ya majumbani kwa ajili ya kupikia.

Alisema, Serikali imeweka wazi na mfumo rafiki wa uwekezaji nchini ili kila mwekezaji aweze kuwekeza katika sekta husika ili kutimiza azma ya Serikali inayotaka 80% ya watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia ndani ya kipindi cha miaka kumi.

"Tunaendelea na mpango mkakati wa miaka kumi, kwa kuweka sheria, kanuni na taratibu ili ikifika mwaka 2034, tuhakikishe watanzania zaidi ya 80% wawe wanatumia nishati ya kupikia na mipango hiyo inaendelea vizuri sana", alisema Mramba.

Alifafanua kuwa, takwimu zinaonyesha kuwa watu 32,000 wanafariki kila mwaka nchini Tanzania kutokana na kutumia nishati isiyo salama kwa kupikia, hivyo katika kukabiliana na changamoto hiyo Serikali inashirikiana na wadau kuhamasiha watanzania kutumia nishati safi ya kupikia kwa kuwawekea mifumo rahisi na rafiki.

Aliwataka wafanyabiashara hao kutanua wigo wa biashara hiyo hadi vijijini na kwa gharama nafuu, ili kila mtanzania aweze kumudu gharama hizo.

Kwa upande wake Mwenyekiti Mteule wa Umoja huo, Benoit Araman ambaye pia ni Mkurugenzi Mkuu wa Oryx Energies Tanzania aliishukuru Serikali ya Awamu ya 6, inayoongozwa na Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mkazo katika matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Araman alisema wao kama wadau wakuu wa kusambaza gesi za mitungi majumbani hapa nchini wanaihakikishia Serikali kuwa wako tayari na wamejipanga kuhakikisha bidhaa hiyo inawafikia watanzania wote tena kwa gharama nafuu na kuboresha njia za upatikanaji wake.

Umoja huo unaundwa na Kampuni 6 zinazofanya biashara ya gesi za mitungi kwa matumizi ya majumbani ambazo ni CAMGAS, O-GAS, LAKE GAS, TAIFA GAS, ORYX GAS na MANJI GAS.



*Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Umoja wa Wafanyabiashara wa Gesi za Mitungi ya Majumbani nchini (TZLPGA) uliofanyika Machi 15, 2023 jijini Dar es Salaam.*




*Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (kushoto) akimueleza jambo Mwenyekiti Mteule wa Umoja wa Wafanyabiashara wa Gesi za Mitungi ya Majumbani nchini (TZLPGA), Benoit Araman( wa pili kulia) wakati akizindua umoja huo uliofanyika Machi 15, 2023 jijini Dar es Salaam.*

# KAMATI YA BUNGE YAWATAKA WANANCHI KULINDA MIUNDOMBINU YA UMEME



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (katikati) akizungumza na Wananchi wa Kata ya Mswaha iliyopo Wilaya ya Korogwe, wakati wa ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme Vijijini inayosimamiwa na wakala wa Nishati Vijijini (REA), Machi 15, 2022.*



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Dunstan Kitandula (katikati) akizungumza na Wananchi wa Kata ya Mswaha iliyopo Wilaya ya Korogwe, wakati wa ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme Vijijini inayosimamiwa na wakala wa Nishati Vijijini (REA), Machi 15, 2022.*

**Na Timotheo Mathayo, Korogwe.**

Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imewataka wananchi kulinda miundombinu ya umeme katika maeneo yenye miradi ya kusambaza umeme inapotekelezwa ili kuepuka vitendo vya hujuma na ubadhilifu wa vifaa kama nyaya, nguzo, mashine umba na vifaa vinginevyo.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dunstan Kitandula wakati wa ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu, mzunguko wa pili inayosimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Ziara hiyo ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilifanyika Machi 15, 2022 katika Kata ya Mswaha pamoja na Chekelei zilizopo wilayani Korogwe katika Mkoa wa Tanga, lengo likiwa ni kupima kama fedha iliyotolewa na Serikali kutekeleza miradi inatumika kwa kiwango kilichokusudiwa.

"Wananchi mnatakiwa kulinda miundombinu ya Umeme kwa wivu mkubwa na mkiona mtu anafanya uharibifu basi toeni taarifa kwenye mamlaka za Serikali zilizopo karibu yenu," Alisema Kitandula.

Aliongeza kuwa "Serikali inawekeza fedha nyingi ili kuhakikisha kila mtanzania anapata huduma ya umeme wa uhakika bila kujali umbali aliopo."

Alipokuwa akizungumza na waandishi wa Habari, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, pia alisema kuwa Serikali imetoa zaidi ya sh. bilioni 12 ili kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika Wilaya ya Korogwe na gharama za kuunganishiwa umeme kwa wananchi wanaoishi vijijini ni sh. 27,000

Pia, Byabato alisema kuwa wilaya ya Korogwe ina jumla ya Kata 40, Vijiji 125 na Vitongoji 645, hivyo jumla ya vijiji 80 vimepata umeme kati ya 125 sawa na asilimia 64 na Vitongoji vilivyopata umeme ni 334 kati ya 645, sawa na asilimia 52.

Alisema kuwa jumla ya Vijiji 45 vilivyobaki vitapata umeme kupitia mradi wa (REA-3) mzunguko wa pili unaoendelea kutekelezwa na Vitongoji 266 vilivyobaki vitapata umeme katika mradi wa kuunganisha umeme kwenye vitongoji vyote Tanzania Bara.

Pia katika ziara hiyo, Wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini walishiriki katika zoezi la kuwasha umeme katika vijiji vya Mswaha na Chekelei vilivyopo katika Wilaya ya Korogwe ambavyo vilikuwa havijapata umeme wa uhakika kupitia miradi ya umeme inayosimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA).



*Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe.Philipo Mulugo akizindua huduma ya umeme katika kijiji cha Mswaha mara baada ya kijiji hicho kufikiwa na huduma ya umeme wa uhakika, Machi 15, 2022.*

# KAMATI YARIDHISHWA NA UTEKELEZAJI UJENZI WA BOMBA LA MAFUTA



*Mwenyekiti wa kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula (wa tatu kushoto) akiwa na wajumbe wa kamati hiyo walipotembelea Kijiji cha Changoleani, Kata ya Mabanda mkoani Tanga ili kukagua utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki linalojengwa kutoka Tanga hadi nchini Uganda, Machi 16,2023.*

**Na Timotheo Mathayo, Tanga**

Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa Mradi wa Bomba la Mafuta ghafi la Afrika Mashariki linalojengwa kutoka nchini Uganda hadi Tanga, Tanzania lenye urefu wa kilomita 1,443.

Mwenyekiti wa kamati hiyo ya Bunge, Dunstan Kitandula amekiri kuridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi huo wakati wa ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi huo wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kwa upande wa Tanzania.

Kamati hiyo ilifika katika kijiji cha Changoleani Machi 16,2023 ili kukagua utekelezaji wa mradi huo wa Bomba la Mafuta Ghafi ambalo nchi za Tanzania na Uganda ni wabia wa mradi.

"Kamati imefika hapa mkoani Tanga katika kijiji cha Changoleani ili kujiridhisha na kasi ya utekelezaji wa ujenzi wa Bomba la Mafuta kwa kuwa Serikali ya Tanzania ni wabia kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na inamiliki asilimia 15 katika mradi wakati wenzetu wa Uganda wanamiliki asilimia 15, na asilimia 70 zilizobaki ni za mwekezaji," alisema Kitandula.

"Kupitia umiliki huu Bunge liliidhinisha fedha ya ujenzi wa mradi, hivyo kamati imefika hapa ili kuona matumizi ya fedha hizo na baada ya kamati kutembelea eneo la mradi imebaini kuwa maandalizi ya ujenzi wa gati yamekamilika na wakandarasi wapo tayari kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo," alieleza Kitandula.

Kitandula aliishauri Serikali kuendelea kusimamia na kufuatilia kwa karibu ujenzi wa mradi huo ambao bomba hilo la mafuta ghafi litapita katika Mikoa minane ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga ili uweze kukamilika kwa wakati.

Akizungumza na Waandishi wa Habari wakati wa ziara hiyo, Mratibu wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta ghafi (EACOP), Asiadi Mrutu alisema kuwa mradi huo umeinua uchumi wa wananchi hasa kwa mikoa yote ambayo mradi huo unatekelezwa kwa kuwa watu zaidi ya 400 wamepata ajira za muda na kudumu, wazawa wakiwa ni 350 na 50 wanatoka nje ya nchi.

Mrutu alisema licha ya upatikanaji wa ajira za kutosha, pia itaimarisha mahusiano baini ya Tanzania na Uganda kwa kuwa mradi huu unatekelezwa na Nchi hizo mbili.

Kuhusu ulipaji wa fidia kwa wanaohama kupisha ujenzi wa bomba hilo, Kamati ilielezwa kuwa fidia kwa wananchi wanaopisha ujenzi huo imetolewa na inaendelea kutolewa bila matatizo na hadi Machi 8, 2023 jumla ya watu 9,276 walikuwa wamesaini mikataba ya fidia.

Kati yao watu 8,479 sawa na asilimia 91.4 wamelipwa fidia na wengine 232 waliobaki wanaendelea kupatiwa elimu na kusainishwa mikataba ya fidia.

Ziara hiyo ilihudhiriwa na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato pamoja na watendaji wengine kutoka Wizara ya Nishati pamoja na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).



*Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba (wa tano kulia) akiwa katika picha pamoja na Mwenyekiti wa kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula (wa nne kulia) na wajumbe wa kamati hiyo walipofika ofisini kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga kwa ajili ya kutembelea Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta.*



*Baadhi ya Miundombinu inayoendelea kuwekezwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi mkoani Tanga katika Kijiji cha Chongoleani.*



*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakiwa pamoja na watendaji mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) katika Kijiji cha Chongoleani mkoani Tanga, mahali lilipo jiwe la Msingi wa Mradi huo, Machi 16,2023.*

# KAMATI YARIDHISHWA UTEKELEZAJI MRADI WA KUZALISHA UMEME KINYEREZI I EXTENSION



*Wabunge wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula (wa nne kulia) akiwa na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato ( wa tano kulia) pamoja na Watendaji kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la umeme Tanzania wakifanya ukaguzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi I extension.*



*Wajumbe kutoka Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakiwa kwenye Moja ya Mtambo wa Kuzalisha umeme kwa kutumia Gesi katika mradi wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi I extension.*

**Na Timotheo Mathayo, Dar es Salaam.**

Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeridhishwa na utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi I extension unaotegemea kuzalisha megawati 185 utakapokamilika.

Mradi huo ulianzishwa ili kuongeza uwezo na kuzalisha umeme katika kituo cha Kinyerezi I chenye uwezo wa kufua Megawati 150 za umeme kwa lengo la kuimarisha gridi ya Taifa.

Mwenyekiti wa kamati hiyo ya Bunge, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Machi 18,2023 aliipongeza Serikali kwa jitihada mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa ili kuhakikisha nchi inapata umeme wa kutosha kwa ajili ya kuwezesha shughuli mbalimbali za uzalishaji.

Kukamilika kwa kituo hicho kutaongeza uzalishaji wa umeme kiasi cha kufikia megawati 335 katika kituo cha Kinyerezi I.

Alisema kuwa baada ya kamati kufanya ukaguzi ilibaini kuwa mitambo mitatu ya kuzalisha umeme imefungwa na kazi ya kukamilisha mtambo uliobaki inaendelea vizuri ili kuwezesha kituo hicho kuzalisha megawati 185 za umeme kutokana na Gesi.

"Mradi huu utapunguza changamoto ya upatikanaji wa umeme nchini, Serikali kupitia Shirika la umeme Tanzania (TANESCO) inatakiwa kuongeza kasi ya usimamizi wa mradi huo ili uweze kukamilika kwa wakati," alisema Kitandula.

Naye, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato alisema mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 kwa Dola za Marekani Milioni 188 sawa na sh. Bilioni 435.48.

"Serikali imelipa Dola za Marekani Milioni 154 ikiwa ni sawa na asilimia 82 ya gharama yote ya mradi na mkandarasi mjenzi wa mradi huo ni Kampuni ya CSI Energy Group Tanzania Limited," alisema Byabato.

Pia, Kamati ya kudumu ya Nishati na Madini ilifanya ziara ya kutembelea na kukagua miundombinu ya Gesi Asilia na usambazaji wa Gesi Asilia nchini inayotekelezwa na Shirikala Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC) chini ya kampuni ya Gesi (GASCO).

Akizungumza mbele ya kamati hiyo, Mhandisi Baltazari Thomas kutoka Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania alisema kuwa uchakataji wa gesi




*Baadhi ya maafisa kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la umeme Tanzania wakiwa kwenye Mtambo wa kuzalisha umeme wa kinyerezi I extension.*

# KAMATI YARIDHISHWA UTEKELEZAJI MRADI WA KUZALISHA UMEME KINYEREZI I EXTENSION

ghafi unafanyika katika mitambo miwili iliyopo Madimba mkoani Mtwara na Songo Songo Mkoani Lindi, ambayo hupokea gesi ghafi kutoka kwa wazalishaji wa mkondo wa juu na gesi asilia inayochakatwa na kusafirishwa hadi Dar es Salaam kupitia bomba kuu la kusafirisha gesi asilia na baadae kusambazwa kwa wahitaji.

Baada ya wajumbe kutembelea na kukagua miundombinu hiyo, wamepongeza Serikali kwa kuendelea kuwekeza katika miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ya usafirishaji wa gesi asilia pamoja na Mradi wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi 1 extension.





*Muonekano wa mitambo mbalimbali inayotumika kuzalisha umeme katika kituo hicho.*



*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakiwa na Watendaji mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati pamoja na Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania wakifanya ukaguzi wa miundombinu ya kusafirisha Gesi asilia.*



*Muonekano wa miundombinu ya kusafirisha Gesi asilia katika kituo cha Kinyerezi kilichopo Jijini Dar es Salaam.*

# KATIBU MKUU WIZARA YA NISHATI AIPONGEZA JAPAN KWA KUENDELEZA USHIRIKIANO KATIKA SEKTA YA GESI NCHINI



*Katibu Mkuu wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (wa kwanza kushoto), akiwa na Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Nishati, Madini na Miundombinu, Matsuda Hiroyuki kutoka JICA, wakati wa tukio la utiaji saini makubaliano ya utekelezaji wa Mradi wa kuhamasisha Matumizi ya Gesi Asilia kati ya Wizara ya Nishati na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (JICA).*

**Na.Timotheo Mathayo, Dodoma**

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Felchesmi Mramba ameipongeza Serikali ya Japan kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (JICA) kwa kuendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika uhamasishaji wa matumizi ya Gesi Asilia nchini.

Alisema hayo wakati wa tukio la utiaji saini makubaliano ya utekelezaji wa Mradi wa kuhamasisha Matumizi ya Gesi Asilia kati ya Wizara ya Nishati na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (JICA).

Makubaliano hayo yalifanyika, Machi 08, 2023, Jijini Dodoma na kushuhudiwa na watendaji mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati na taasisi zake akiwemo, Mkurugenzi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC), Bw.Mussa Makame pamoja na Mhandisi Poline Msuya kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji nchini (EWURA) pamoja na watendaji mbalimbali kutoka Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan.

"Lengo la makubaliano haya ni kuifanya Jamii ya Kitanzania kunufaika na rasilimali za gesi zilizopo nchini, ambapo katika kufanikisha jambo hilo Serikali ya Japan ilikubali kusaidia katika eneo la kuhamasisha Matumizi ya Gesi Asilia Nchini, Amesema Mhandisi Mramba.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Nishati, Madini na Miundombinu Matsuda Hiroyuki kutoka Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (JICA), alisema kuwa Serikali ya Japan kupitia mashirika ya maendeleo itaendelea kuwekeza katika miradi mbalimbali ya kimaendeleo ikiwemo sekta ya Gesi nchini ili kuwezesha jamii ya kitanzania kunufaika na Rasimali zilizopo nchini.



*Katibu Mkuu wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (wa kwanza kushoto), akibadilishana hati ya makubaliano na Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Nishati, Madini na Miundombinu, Matsuda Hiroyuki kutoka JICA, mara baada ya tukio la utiaji saini makubaliano ya utekelezaji wa Mradi wa kuhamasisha Matumizi ya Gesi Asilia kati ya Wizara ya Nishati na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (JICA).*



*Mkurugenzi wa Shirika la Petrol Nchini, Bw.Mussa Makame ( wa tatu kushoto),akiwa na Mhandisi Poline Msuya ( wa pili kushoto) kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji nchini Tanzania (EWURA) pamoja na Fakihi Mohamed kutoka Wizara ya Nishati, wakiwa katika tukio la utiaji saini makubaliano ya utekelezaji wa Mradi wa kuhamasisha Matumizi ya Gesi Asilia kati ya Wizara ya Nishati na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (JICA).*



*Watendaji kutosha Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (JICA), wakiwa katika tukio la utiaji saini makubaliano ya utekelezaji wa Mradi wa kuhamasisha Matumizi ya Gesi Asilia kati ya Wizara ya Nishati na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (JICA).*



*Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (katikati), akiwa na Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Nishati, Madini na Miundombinu , Matsuda Hiroyuki kutoka JICA ( wa tatu kulia) pamoja na watendaji mbalimbali walioshiriki tukio la utiaji saini makubaliano ya utekelezaji wa Mradi wa kuhamasisha Matumizi ya Gesi Asilia kati ya Wizara ya Nishati na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (JICA*

# WIZARA YA NISHATI YAPONGEZWA KWA KASI YA USIMAMIZI WA UJENZI KITUO CHA KUPOZA UMEME CHA CHALINZE



*Mwenyekiti wa kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Dunstan Kitandula (katikati) akiwa na Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mh. Judith Kapinga (wa kwanza kulia) wakiwa kwenye kikao na watendaji , kabla ya kuanza kutembelea mradi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Bwawa la Julius Nyerere hadi Chalinze pamoja na Ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme Chalinze.*

**Na. Timotheo Mathayo, Pwani.**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeipongeza Wizara ya Nishati kwa kasi nzuri ya usimamizi wa ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Chalinze.

Pongezi hizo zilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Dunstan Kitandula, Machi 17,2023 wakati Kamati hiyo ilipotembelea Kituo cha Kupoza Umeme cha Chalinze kilichopo Mkoani Pwani.

"Nchi imefanya uwekezaji mkubwa katika Bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere na pindi umeme utakapoanza kuzalishwa utaletwa hapa kwenye kituo cha Chalinze na kuingizwa kwenye Gridi ya Taifa," alisema Kitandula.

"Hivyo kila mmoja anapaswa kujua kwamba mradi huu ni muhimu kwani ujengaji wake unatakiwa kwenda sambamba na utekelezaji wa Mradi wa kuzalisha umeme," aliongeza Kitandula.

Akizungumza na Waandishi wa Habari wakati wa ziara hiyo, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato alisema Serikali inatarajia kukamilisha ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Bwawa la Julius Nyerere ambapo njia hiyo ya kusafirisha umeme ina urefu wa kilomita 160 na ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme cha Chalinze unahusisha ufungaji wa Transfoma Sita.

"Mradi unagharamiwa na Serikali ya Tanzania, gharama ya mradi ni Dola za Marekani milioni 51.5 na sh. bilioni 39.12 ambapo ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme utatumia Dola za Marekani Milioni 44.06 na sh. Bilioni 30.85 zinatumika kwa ajili ya kujenga kituo cha kupoza umeme cha Chalinze," alisema Byabato.

Wakili Byabato amemtaja Mkandarasi mjenzi wa mradi huo wa kusafirisha umeme kuwa ni Larsen & Toubro Limited kutoka India na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze unatekelezwa na Mkandarasi TBEA kutoka China.

Naye, Meneja Msimamizi wa mradi huo, Mhandisi Newton Mwakifwamba alisema mradi upo katika hatua mbalimbali ya utekelezaji ambapo njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 imefikia asilimia 92.

Ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze unaohusisha ufungaji wa mashine umba sita umefikia asilimia 55 na kasi ya ujenzi inaendelea vizuri.

Baadhi ya viongozi walioshiriki katika ziara hiyo ni Kaimu Kamishina Msaidizi wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Christopher Bitesigirwe, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande pamoja na Watendaji wengine.



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizungumza na wajumbe wa kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini (hawapo pichani) wakati walipofika katika eneo la mradi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Bwawa la Julius Nyerere hadi Chalinze pamoja na Ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme Chalinze.*




*Mkurugenzi mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Maharage Chande akizungumza jambo wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kutembelea mradi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Bwawa la Julius Nyerere hadi Chalinze pamoja na Ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme Chalinze.*



*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Watendaji kutoka Wizara ya Nishati pamoja na Shirika la Umeme Tanzania wakikagua ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Bwawa la Julius Nyerere hadi Chalinze pamoja na Ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme Chalinze.*



*Muonekano wa Ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme cha Chalinze pamoja na baadhi ya Miundombinu ikiwemo mashine umba (Transfoma), zitakazotumika katika ujenzi wa mradi huo.*

**JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**





***Fika Ofisi ya Mawasiliano,***

Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au

Wasiliana nasikwa **simu namba:** +255-26-2322018

**Nukushi:** +255-26-2320148

*Wizara ya Nishati* *@nishati2017* *Wizara_ya_nishati_tanzania* *www.nishati.go.tz*